




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



*Dar es Salaam, 20 Septemba, 2023*

## TAARIFA KWA UMMA

### KUKAMILIKA KWA AWAMU YA PILI NA KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

#### 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na wadau wa Elimu ya Juu ndani na nje ya Tanzania kuwa Awamu ya Pili ya udahili wa Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2023/2024 imekamilika. Majina ya waliodahiliwa katika awamu hii yanatangazwa na vyuo husika.

#### 2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Kwanza na ya Pili wanahimizwa **kuthibitisha** udahili wao katika chuo kimojawapo **kuanzia tarehe 25 hadi 30 Septemba, 2023** kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Aidha, inasisitizwa kuwa uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Orodha ya majina ya waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU ([www.tcu.go.tz](http://www.tcu.go.tz)).

#### 3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI 2023/2024

Tume inatangaza kuwa Awamu ya Tatu ya udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2023/2024 itaanza tarehe 25 hadi 29 Septemba, 2023. Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakuweza kupata nafasi za kudahiliwa katika awamu zilizopita kutokana na sababu mbalimbali, watumie fursa hii vizuri kwa kutuma maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda.

Aidha, Tume inaelekeza Taasisi za Elimu ya Juu nchini kutangaza programu ambazo bado zina nafasi. Waombaji udahili na vyuo wanahimizwa kuzingatia utaratibu wa udahili wa Awamu ya Tatu kama ulivyooneshwa kwenye kalenda ya udahili iliyoko katika tovuti ya TCU ([www.tcu.go.tz](http://www.tcu.go.tz)).

#### **4.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI**

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

#### **5.0 TAHADHARI**

TCU inawaasa wananchi kuepuka kutapeliwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

**KATIBU MTENDAJI**

**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**